

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA MJINI MOSHI



KUKATIKA KWA MAJI SAFI

Wakati Mamlaka imedhamiria kutoa Huduma ya Maji Safi na Maji Taka kwa Wakazi wa Mji wa Moshi kwa muda wote wa Masaa 24 (Ishirini na nne), matatizo yasiyowezakuzuilika yanaweza kusababisha nia hii nzuri kutotimizwa.

Kukatika kwa Huduma ya Maji Safi katika Eneo ama Nyumba ya Mteja kunaweza kusababishwa na mambo makuu yafuatayo:-

- **Mteja husika Kutolipia Deni lake la Matumizi ya Maji Safi kwa muda wa Miezi Miwili Mfululizo**
- **Mteja husika Kutolipia Deni lake la Matumizi ya Huduma ya Maji Taka kwa muda wa Miezi Miwili Mfululizo**
- **Mteja husika kuharibu Dira Yake ya Maji ama Viungio vingine katika Bomba la Mteja na hivyo kusababisha Uvujaji wa Maji**

- Kupasuka ama kuwa na Uvujaji wa Maji na hitilafu yoyote kwenye Bomba inayopeleka Maji Safi kwenye Makazi ya Mteja
- Kupasuka kwa Bomba Kuu za Kusambazia Maji, ama hitilafu katika Vyanzo, Matangi ya Kuhifadha Maji au Mtandao wa Bomba za Maji na kadhalika,

MAMBO YA KUZINGATIA:

- Lipia Huduma unayoipata ya Maji Safi na Maji Taka kuanzia tarehe 1 hadi 15 ya kila mwezi,
- Toa Taarifa na Fanyia Matengenezo Bomba zako mara tuu kunapokuwa na uvujaji,
- Toa Taarifa kila mara unapoona Bomba Kuu za Kusambazia Maji zimepasuka na zinavuja.

Kwa kufanya hivyo, utakuwa unaboresha na kuhakikisha kuwa huduma hizi muhimu zinaendelea kuwepo kwa faida yetu sote!

**MKURUGENZI MTENDAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA
MJINI MOSHI**

**S.L.P 324, MOSHI Simu: 2751164
Barua Pepe: muwasa@kilionline.com**